© Quran wa Sunnah Society of East Africa – E-books 2005. www.qssea.net

Asili: Gazeti la chuo kikuu cha ki-Islamu cha Madeenah (Toleo la Pili la mwaka wao wa Nne) Shawaal 1391H

Kutokana na Rehma na Ukarimu wa Mwenyezi Mungu juu ya waja wake na kutokana na fadhla zake juu yao ni kwamba aliwapelekea mjumbe aliyetokamana nao ili awafikiliziye ujumbe utokao kwa Mola wao na kuwaongoza katika kila kitu ambacho kitakacho wafaidisha wao na kuwaonya kutokamana na kila kitu chenye kuwaletea madhara. Na kwa hakika, Mtume Muhammad (*Sallallaahu 'alayhi wasallam*) alitekeleza jukumu lake la kuufikiliza ujumbe kwa njia ya ukamilifu na iliyotimia - kwahivyo, aliwaongoza Umma wake juu ya kila kilicho kizuri na akawaonya dhidi ya kila jambo ovu. Mwenyezi Mungu alimchagulia pote la watu waliokuwa ni bora wa taifa hili, ili washirikiana nae na kujifunza ilimu kutoka kwake. Nalo lilikuwa ni pote ambalo lenyewe lilikuwa bora kuliko mataifa yote. Kwahivyo, Mwenyezi Mungu aliwatukuza kwa kuwaruhusu wao kuwa (au kushirikiana) pamoja na Mtume Wake. Aliwahusisha wao makhsusi katika haya maisha ya kilimwengu kwa kumuona yeye na kusikiliza hadeeth zake moja kwa moja kutoka katika kinywa chake kitakatifu. Hizi ni fadhla za Mwenyezi Mungu, ambazo Humpa amtakae. Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa Fadhla.

Na kwa hakika Maswahaba waliufikiliza ujumbe kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu ambao aliotumilizwa nao wa uongofu juu ya njia ya ukamilifu iliyo sawa. Kwahivyo wao watastahiki malipo bora zaidi kutokana na usuhuba wao na Mtume wa Mwenyezi Mungu, kupigana kwao kwenye Jihaad pamoja nae na kujitolea kwa vitendo vyao katika kuusambaza Uislamu.

Na vilevile watastahiki malipo sawa kama wale waliokuja baada yao kwa vile wao walikuwa ni kama wajumbe baina yao na Mtume wa Mwenyezi Mungu. Hii ni kwa sababu: **"Yeyote mwenye kulingania katika uongofu, atapata malipo mfano wa malipo ya wale watakaoufuata uongofu ule baada yake. Na wala haitopunguza kitu chochote kutoka katika malipo yao."**[1] Hili ni jambo lililothibitishwa na Mtume (*Sallallaahu 'alayhi wasallam*) katika hadeeth iliyopokewa na Imaam Muslim katika saheeh yake. Mwenyezi Mungu (*Subhaanahu wata'aalah*) amewasifu katika kitabu chake kitakatifu na Mtume wa Mwenyezi Mungu (*Sallallaahu 'alayhi wasallam*) nae akawasifu katika Sunnah zake zilizotahirika. Na jambo hili linawatosheleza wao kabisa kuwa ni wema na heshima iliyo kubwa mno.

Akasema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wata'aalah):

[1] **Hadeeth Saheeh:** Imepokewa na Muslim (2674), Abu Dawood (4609), At-Tirmidhee (2676), Ibn Maajah (206) na wengineo.

© Quran wa Sunnah Society of East Africa – E-books 2005. www.qssea.net

وَٱلسَّٰبِقُونَ ٱلْأَوَّلُونَ مِنَ ٱلْمُهَٰجِرِينَ وَٱلْأَنصَارِ وَٱلَّذِينَ ٱتَّبَعُوهُم بِإِحْسَٰنٍ
رَّضِىَ ٱللَّهُ عَنْهُمْ وَرَضُوا۟ عَنْهُ وَأَعَدَّ لَهُمْ جَنَّٰتٍ تَجْرِى تَحْتَهَا ٱلْأَنْهَٰرُ
خَٰلِدِينَ فِيهَآ أَبَدًا ۚ ذَٰلِكَ ٱلْفَوْزُ ٱلْعَظِيمُ ﴿١٠٠﴾

Na wale walio tangulia, wa kwanza, katika Wahajiri na Ansari, na walio wafuata kwa wema, Mwenyezi Mungu ameridhika nao, na wao wameridhika naye; na amewaandalia Bustani zipitazo mito kati yake, wadumu humo milele. Huko ndiko kufuzu kukubwa.[1]

Na akasema:

مُّحَمَّدٌ رَّسُولُ ٱللَّهِ ۚ وَٱلَّذِينَ مَعَهُۥٓ أَشِدَّآءُ عَلَى ٱلْكُفَّارِ رُحَمَآءُ بَيْنَهُمْ ۖ
تَرَىٰهُمْ رُكَّعًا سُجَّدًا يَبْتَغُونَ فَضْلًا مِّنَ ٱللَّهِ وَرِضْوَٰنًا ۖ سِيمَاهُمْ فِى
وُجُوهِهِم مِّنْ أَثَرِ ٱلسُّجُودِ ۚ ذَٰلِكَ مَثَلُهُمْ فِى ٱلتَّوْرَىٰةِ ۚ وَمَثَلُهُمْ فِى ٱلْإِنجِيلِ
كَزَرْعٍ أَخْرَجَ شَطْـَٔهُۥ فَـَٔازَرَهُۥ فَٱسْتَغْلَظَ فَٱسْتَوَىٰ عَلَىٰ سُوقِهِۦ يُعْجِبُ
ٱلزُّرَّاعَ لِيَغِيظَ بِهِمُ ٱلْكُفَّارَ ۗ وَعَدَ ٱللَّهُ ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ وَعَمِلُوا۟ ٱلصَّٰلِحَٰتِ
مِنْهُم مَّغْفِرَةً وَأَجْرًا عَظِيمًۢا ﴿٢٩﴾

29. Muhammad ni Mtume wa Mwenyezi Mungu. Na walio pamoja naye wana nguvu mbele ya makafiri, na wanahurumiana wao kwa wao. Utawaona wakiinama na kusujudu wakitafuta fadhila na radhi za Mwenyezi Mungu. Alama zao zi katika nyuso zao, kwa athari ya kusujudu. Huu ndio mfano wao katika Taurati. Na mfano wao katika Injili ni kama mmea ulio toa chipukizi lake, kisha ukalitia nguvu, ukawa mnene, ukasimama sawa juu ya ubuwa wake, ukawafurahisha wakulima, ili kuwakasirisha kwa ajili yao makafiri. Mwenyezi Mungu amewaahidi walio amini na wakatenda mema katika wao msamaha na ujira mkubwa.[2]

Katika maneno ya Mwenyezi Mungu kuhusu maswahaba: "yakwamba huwakasirisha kwa ajili yao makafiri", kunapatikana humo maonyo, na

[1] Soorah at-Tawbah 9:100
[2] Soorah al-Fat'h 48:29

© Quran wa Sunnah Society of East Africa – E-books 2005. www.qssea.net
vitisho vikali, na kuhadharishwa kuovu mno juu ya wale wanaoghadhibishwa na maswahaba au wale wenye chuki juu yao katika nyoyo zao.

Akasema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wata'aalah):

وَمَا لَكُمْ أَلَّا تُنفِقُوا۟ فِى سَبِيلِ ٱللَّهِ وَلِلَّهِ
مِيرَٰثُ ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضِ ۚ لَا يَسْتَوِى مِنكُم مَّنْ أَنفَقَ مِن
قَبْلِ ٱلْفَتْحِ وَقَٰتَلَ ۚ أُو۟لَٰٓئِكَ أَعْظَمُ دَرَجَةً مِّنَ ٱلَّذِينَ أَنفَقُوا۟ مِنۢ بَعْدُ
وَقَٰتَلُوا۟ ۚ وَكُلًّا وَعَدَ ٱللَّهُ ٱلْحُسْنَىٰ ۚ وَٱللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرٌ ﴿١٠﴾

10. Na mna nini hata hamtoi katika Njia ya Mwenyezi Mungu, na hali urithi wa mbingu na ardhi ni wa Mwenyezi Mungu? Hawawi sawa miongoni mwenu wenye kutoa kabla ya Ushindi na wakapigana vita. Hao wana daraja kubwa zaidi kuliko wale ambao walio toa baadae na wakapigana. Na wote hao Mwenyezi Mungu amewaahidia wema. Na Mwenyezi Mungu anazo khabari za mnayo yatenda.[1]

Kuhusu kuzigawanya ngawira (ghanima), Mwenyezi Mungu akasema:

لِلْفُقَرَآءِ ٱلْمُهَٰجِرِينَ ٱلَّذِينَ أُخْرِجُوا۟ مِن دِيَٰرِهِمْ وَأَمْوَٰلِهِمْ يَبْتَغُونَ
فَضْلًا مِّنَ ٱللَّهِ وَرِضْوَٰنًا وَيَنصُرُونَ ٱللَّهَ وَرَسُولَهُۥٓ ۚ أُو۟لَٰٓئِكَ هُمُ
ٱلصَّٰدِقُونَ ﴿٨﴾

وَٱلَّذِينَ تَبَوَّءُو ٱلدَّارَ وَٱلْإِيمَٰنَ مِن قَبْلِهِمْ يُحِبُّونَ مَنْ
هَاجَرَ إِلَيْهِمْ وَلَا يَجِدُونَ فِى صُدُورِهِمْ حَاجَةً
مِّمَّآ أُوتُوا۟ وَيُؤْثِرُونَ عَلَىٰٓ أَنفُسِهِمْ وَلَوْ كَانَ بِهِمْ خَصَاصَةٌ ۚ وَمَن يُوقَ
شُحَّ نَفْسِهِۦ فَأُو۟لَٰٓئِكَ هُمُ ٱلْمُفْلِحُونَ ﴿٩﴾

[1] AL-Hadyd 57:10

© Quran wa Sunnah Society of East Africa – E-books 2005. www.qssea.net

وَٱلَّذِينَ جَآءُو مِنۢ بَعۡدِهِمۡ يَقُولُونَ رَبَّنَا ٱغۡفِرۡ لَنَا وَلِإِخۡوَٰنِنَا ٱلَّذِينَ سَبَقُونَا
بِٱلۡإِيمَٰنِ وَلَا تَجۡعَلۡ فِي قُلُوبِنَا غِلّٗا لِّلَّذِينَ ءَامَنُواْ رَبَّنَآ إِنَّكَ رَءُوفٞ
رَّحِيمٌ ١٠

Wapewe mafakiri Wahajiri walio tolewa majumbani mwao na mali yao kwa ajili ya kutafuta fadhila kutoka kwa Mwenyezi Mungu na radhi zake, na wanamsaidia Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Hao ndio wa kweli. Na walio na maskani zao na Imani yao kabla yao, wanawapenda walio hamia kwao, wala hawaoni choyo katika vifua vyao kwa walivyo pewa (Wahajiri), bali wanawapendelea kuliko nafsi zao, ingawa wao wenyewe ni wahitaji. Na mwenye kuepushwa uchoyo wa nafsi yake, basi hao ndio wenye kufanikiwa. Na walio kuja baada yao wanasema: Mola wetu Mlezi! Tughufirie sisi na ndugu zetu walio tutangulia kwa Imani, wala usijaalie ndani ya nyoyo zetu undani kwa walio amini. Mola wetu Mlezi! Hakika Wewe ni Mpole na Mwenye kurehemu.[1]

Aya ya kwanza katika aya hizi tatu kutoka katika Soorah al-Hashr zinawahusu Muhaajireen (Maswahaba **waliohama** kutoka Makkah hadi Madeenah). Aya ya pili inawahusu Ansaar (Maswahaba waliokuwa ni wakaazi wa Madeenah ambao ndiwo **waliowasaidia** na kuwahami Muhaajireen). Aya ya tatu inawahusu wale watakaokuja baada ya Muhaajireen na Ansaar, na wale wanaowaombea wao msamaha, na kumuomba Mwenyezi Mungu asiwatie chuki za kuwachukia maswahaba katika nyoyo zao. Na hapana chochote cha zaidi mbali na makundi haya matatu isipokuwa kwa yule mwenye kujitenga nao (hao maswahaba) na kutumbukia ndani ya mojawapo ya mitego ya Shetani. Hii ndiyo sababu ya 'Aa'ishah (radhiallaahu 'anha) kumwambia 'Urwah Ibn Az-Zubair kuhusu hali za baadhi ya wale waliojitenga nao wakasahauliwa:

"Waliamrishwa kuwaombea msamaha (maghfira) maswahaba wa mtume wa Mwenyezi Mungu, lakini (badala yake) wao wakawakadhibisha." Akaipokea riwaya hii Imaam Muslim kwenye sehemu ya mwisho ya Saheeh yake. An-Nawawee akasema katika kuifafanua riwaya hiyo, baada ya kuitaja ayah katika Soorah al-Hashr, yakwamba:

"Imaam Maalik alitumia (riwaya) hii kuwa ni ushahidi wa hukmu yake yakwamba yoyote mwenye kuwakadhibisha maswahaba hastahiki kupata ngawira (ghanima). Hii ni kwa sababu Mwenyezi Mungu aliikusudia (mali hiyo) kwa wale wenye kuwaombea maghfira peke yao wakiwemo miongoni mwa wale waliokuja baada yao."

[1] Soorah al-Hashr: 57:8-10

© Quran wa Sunnah Society of East Africa – E-books 2005. www.qssea.net

Ibn Katheer akasema kwenye tafsiri yake ya aya hii:

"Ni hukmu iliyoje ya Imaam Maalik iliyotokamana na aya hii, ambayo ndani yake Raafidhee – yule mwenye kuwakadhibisha maswahaba – hana sehemu ya pato la ngawira, kwa ajili ya ukosefu wake wa kujinasibisha na sifa za wale waliosifiwa na Mwenyezi Mungu katika maneno yake: **"Mola wetu Mlezi! Tughufirie sisi na ndugu zetu walio tutangulia kwa Imani, wala usijaalie ndani ya nyoyo zetu undani kwa walio amini. Mola wetu Mlezi! Hakika Wewe ni Mpole na Mwenye kurehemu."**

Mtume Muhammad (*Sallallaahu 'alayhi wasallam*) amesema: **"Wabora wa watu ni (wa) karne yangu, kisha ni wale waliokuja baada yao, na kisha ni wale waliokuja baada ayo."**[1] Imepokewa na Imaam Al-Bukhaaree, Muslim na wengineo kutoka katika riwaya ya 'Imraan Ibn Husayn na 'Abdullaah Ibn Mas'ood, Mwenyezi Mungu Awe radhi nao wote wawili. Muslim aliipokea kutoka kwa Abu Hurairah na maneno yasemayo: **"Walio bora miongoni mwa Taifa langu (Ummah) ni karne niliyotumilizwa kwayo – kisha ni wale watakaokuja baada yao na kisha ni wale watakaokuja baada yao."** Inamuelea zaidi Mwenyezi Mungu iwapo alilitaja kundi la tatu au hakulitaja. Vilevile Muslim akapokea kutoka kwa 'Aaishah yakwamba alisema: "Siku moja mtu fulani alimuuliza Mtume (*Sallallaahu 'alayhi wasallam*): 'Ni watu gani walio bora zaidi?' Nae akajibu: **'Karne ya watu ambao ninaoishi nao (wakati wangu, kisha (karne) ya pili, kisha ya tatu.'"** Imepokewa kwenye Saheeh mbili (ya Bukhaaree na Muslim) kutoka katika riwaya ya Abu Sa'eed Al-Khudree yakwamba Mtume (*Sallallaahu 'alayhi wasallam*) amesema:

"Utawajilia watu wakati ambao kikundi cha watu watapigana (kwenye Jihaad), na itasemwa: 'Pana yoyote miongoni mwenu aliyekuweko pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu?' (yaani: Swahaba) Nao watajibu 'Ndio' kwahivyo watapewa ushindi. Kisha utawajilia watu wakati ambao kikundi cha watu watapigana (kwenye Jihaad), na itasemwa: 'Pana yoyote miongoni mwenu aliyekuweko pamoja na maswahaba wa Mtume wa Mwenyezi Mungu?' (yaani: Taabi'een) Nao watajibu 'Ndio' kwahivyo watapewa ushindi. Kisha utawajilia watu wakati ambao kikundi cha watu watapigana (kwenye Jihaad), na itasemwa: 'Pana yoyote miongoni mwenu aliyekuweko pamoja na waliokuweko na maswahaba wa

[1] **Saheeh Hadeeth:** Imepokewa na Al-Bukhaaree na Muslim kutoka katika hadeeth ya Ibn Mas'ood. Maswahaba wengi waliipokea hadeeth hii, miongoni mwao akiwemo 'Imraan Ibn Husayn na An-Nu'maan Ibn Basheer. Angalia kitabu As-Saheehah cha Imaam Al-Albaanee: (699-700)

© Quran wa Sunnah Society of East Africa – E-books 2005. www.qssea.net

Mtume wa Mwenyezi Mungu?' (yaani: Atbaa' Taabi'een). Nao watajibu 'Ndio' kwahivyo watapewa ushindi."[1]

Akapokea Ibn Battah kwa silsila ya riwaya saheeh – kulingana na Minhaaj As-Sunnah cha Ibn Taymiyyah – kutoka kwa Ibn 'Abbaas (*Radhiallaahu 'anhum*) yakwamba alisema: "Musiwabughudhi maswahaba wa Mtume wa Mwenyezi Mungu, kwani saa moja yenye kutumiwa pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu na mmoja wao ni bora kuliko jambo jema la mmoja wenu (lililotendwa) kwa miaka arubaini."

Kulingana na maneno yaliyonukuliwa kutoka kwa Wakee', amesema: "... bora kuliko jambo jema la mmoja wenu (lililotendwa) katika maisha yake yote."

Na Sa'eed Ibn Zayd (*Radhiallaahu 'anhu*) alipotaja majina ya maswahaba kumi waliopewa bishara njema ya (kuingia) peponi, alisema:

"Naapa kwa jina la Mwenyezi Mungu, kukutana kwa mmoja miongoni mwao na mtume wa Mwenyezi Mungu ni bora kuliko amali za mmoja wenu, hata kama ataitekeleza amali hiyo kwa umri wa mtume Nuh." Hayo yalipokelewa na Abu Dawood na at-Tirmidhee.[2]

Jaabir alihadithia yakwamba: "Siku moja 'Aaisha aliambiwa: 'Kuna baadhi ya watu wanaokusudia kuwakashifu maswahaba wa Mtume wa Mwenyezi Mungu, hata Abu Bakr na 'Umar.' Nae akasema: 'Kwani hayo hayakukuridhisha wewe? Amali zao zimefikiya kikomoni, lakini Mwenyezi Mungu amependezwa yakwamba malipo yao mema yasifike ukingoni.'"

Ibn al-Atheer aliyataja haya katika kitabu chake Jaami'-ul-Usool. Kitu chenye kuonyesha ushahidi wa maneno aliyoyasema ('Aaisha) ni maneno yake Mtume (Sallallaahu 'alayhi wasallam) katika hadeeth iliyo saheeh isemayo: **"Mtu aliyefilisika katika Ummah wangu atakuja siku ya Malipo haliyakuwa ameswali, amefunga, ametoa Zakaat. Lakini (kwa upande mwengine) amemkosea mtu huyu, akamkashifu huyu, akamdhulumu huyu pesa zake, akamuuwa huyu, na akampiga huyu. Kwahivyo baadhi ya amali zake njema atapewa mtu huyu na baadhi atapewa mtu yule. Kwahivyo amali zake njema zikimalizika kabla ya kumaliza madeni ya aliowadhulumu, atabebeshwa kutoka kwenye**

[1] **Saheeh Hadeeth:** Imepokewa na Al-Bukhaaree (6/88 na 610 katika kitabu cha al-fat'h), Muslim (3532), Ahmad (3/7), Al-Humaidee (743), Al-Baghawee katika Sharh-us-Sunnah (14/73-74) kutoka katika njia ya Jaabir Ibn 'Abdillaah nae kutoka kwa Abu Sa'eed Al-Khudree.

[2] **Hasan Hadeeth:** Imepokewa na Abu Dawood (4650), An-Nasaa'ee katika Al-Kubraa, Ibn Maajah (134) na Ahmad (1629).

© Quran wa Sunnah Society of East Africa – E-books 2005. www.qssea.net

madhambi yao ahukumiwe nayo yeye. Na kisha atatupiliwa mbali ndani ya moto wa Jahannam."[1]

AL-Bukhaaree alipokea katika saheeh yake kutoka kwa Abu Sa'eed al-Khudhree (*Radhiallaahu 'anhu*) yakwamba Mtume (*Sallallaahu 'alayhi wasallam*) amesema: **"Musiwabughudhi maswahaba zangu! kwani hata kama mmoja wenu angelijitolea kipimo chenye kulingana na mlima wa Uhud wa dhahabu kwa njia ya sadaka, basi haitokuwa sawa na hata kipimo cha Madd (Mteko mmoja kwa mikono miwili kwa pamoja) ya mmoja wao wala nusu yake."**

Imaam Muslim akapokea katika saheeh yake kutoka kwa Abu Hurairah (*Radhiallaahu 'anhu*) yakwamba Mtume (*Sallallaahu 'alayhi wasallam*) amesema: **"Musiwalaani maswahaba zangu! Musiwalaani maswahaba zangu! kwani naapa kwa yule ambae Aliyeimiliki nafsi yangu, lau kama mmoja wenu angelijitolea (kiwango cha) dhahabu (kilicho na) ukubwa wa mlima wa Uhud kwa njia ya sadaka, basi haitokuwa sawa na hata kipimo cha madd moja ya mmoja wao wala (hata) nusu yake."**

Vilevile akaipokea kutoka kwa Abu Sa'eed (*Radhiallaahu 'anhu*) na maneno yafuatayo:
"Palitokea kutoelewana baina ya Khaalid Ibn Al-Waleed na 'Abdur-Rahmaan Ibn 'Awf, basi Khalid akamshutumu 'Abdur-Rahmaan Ibn 'Awf. Mtume wa Mwenyezi Mungu (*Sallallaahu 'alayhi wasallam*) akasema: "Musimshutumu yoyote miongoni mwa maswahaba zangu. Kwani lau kama mmoja wenu angelijitolea dhahabu ukubwa wa mlima wa Uhud kwa njia ya sadaka, basi haitokuwa sawa na hata kipimo cha madd moja ya mmoja wao wala nusu yake."

Sasa ikiwa Upanga wa Mwenyezi Mungu, Khaalid Ibn Al-Waleed na wengine waliosilimu baada ya mkataba wa Hudaybiyah wameshindwa kuwa na wingi wa amali zao njema zinazoweza kulingana na uchache wa amali zilizofanywa na 'Abdur-Rahmaan Ibn 'Awf na wengineo ambao waliotangulia kusilimu – hata kama wote hao walibahatika kwa kuwa pamoja na Mtume – Sasa jee, huwaje kwa wale ambao hata hawakuifikia heshima ya (kutokamana na) maswahaba ukiwalinganisha na hao watu watukufu? Kwa kweli umbali ni mkubwa na kwa hakika ni tafauti iliyo mbali mno! Hebu linganisha umbali wa ardhi na mbingu, seuze umbali wa tabaka ya saba ya ardhi (iliyo chini zaidi) kutoka tabaka ya saba ya mbingu (iliyo juu zaidi)! Hizi ni fadhila za Mwenyezi Mungu, ambazo humpa Amtakae. Na Mwenyezi Mungu ni mwingi wa Fadhla, asiye na kifani!

---

[1] **Saheeh Hadeeth:** Imepokewa na Muslim (2581), At-Tirmidhee (2418), Ahmad (2/303), Al-Bayhaqee (6/93) kutoka kwenye isnadi ya Al-'Alaa Ibn 'Abdir-Rahmaan kutoka kwa babake nae kutoka kwa Abu Hurairah kwa njia ya marfoo'. At-Tirmidhee alisema ilikuwa ni hasan saheeh

© Quran wa Sunnah Society of East Africa – E-books 2005. www.qssea.net

Hizi ndizo baadhi ya ayaat za Qur'an na Ahaadeeth za Mtume zenye kuonyesha ushahidi wa fadhla walizokuwa nazo hawa wabora wa watu, ambao mifano yao haikuwahi kupatikana kabla na wala hawatowahi kupatikana baadae. Tunamuomba Mwenyezi Mungu Awe radhi nao.

Maswahaba wote wa Mtume wa Mwenyezi Mungu ni watu waaminifu kutokamana na ushahidi walioshuhudiliwa na Mwenyezi Mungu na kutokamana na Sifa Alizowasifu nazo Mwenyezi Mungu na Mtume wake. An-Nawawee amesema katika kitabu chake at-Taqreeb, kilichofafanuliwa na as-Suyootee kwenye kitabu chake Tadreeb Ar-Raawee:

"Maswahaba wote ni watu waaminifu – wale ambao waliohusika kwenye misiba (fitan) na wale wasiokuwa wao – kulingana na muafaka wa Wanavyuoni."

Al-Haafidh Ibn Hajr amesema katika Al-Isaabah: "Ahl-us-Sunnah wamekubaliana bila ya upinzani wowote yakwamba (maswahaba) wote ni waaminifu na hapana yoyote apingae jambo hili isipokuwa baadhi ya wapotofu miongoni mwa wazushi."

Hii ndiyo sababu hapana madhara yoyote kwa kutojulikana swahaba kwenye silsila ya upokezi wa riwaya. Kwahivyo iwapo Taabi'ee atasema: "Imepokewa na mtu aliyekuwa ameandamana na Mtume…" jambo hili halidhuru riwaya hiyo. Hii ni kwa sababu kutomjua swahaba (katika silsila ya upokezi) hakudhuru kitu kwa vile wao wote ni waaminifu. Al-Khateeb Al-Baghdaadee amesema katika kitabu chake Al-Kifaayah:

"Kila hadeeth yenye silsila ya upokezi wa riwaya iliyounganishwa baina ya aliyepokea na Mtume isitumiwe mpaka kwanza ikubaliwe kuhusu ukweli na uaminifu wa watu wake (katika silsila). Na ni wajibu kufanya uchunguzi kuhusu hali zao, isipokuwa Sahaabee (maswahaba) ambao walioipokea (au wakaielekeza hadeeth yenyewe) kutoka kwa Mtume. Hii ni kwa sababu uaminifu wa maswahaba ni jambo lililothubutu na lenye kujulikana kutokana na uthibitisho wa Mwenyezi Mungu kwao wao na kutujulisha sisi kuhusu hali yao ya Utakaso na fadhila Zake juu yao zilizoko kwenye maandishi ya Qur'aan…"

Kisha akaendelea kuzipanga baadhi ya ayaat na ahaadeeth zinazohusu wema wao na kisha akasema:

"Na hata kama Mwenyezi Mungu au Mtume wake (*Sallallaahu 'alayhi wasallam*) hangetaja chochote kuwahusu wao katika yale ambayo tuliyowatajia hivi sasa (katika wema waliokuwa nao), hali waliyokuwa nayo ya kufanya Hijrah, kupigana vita vya Jihaad, au kujitolea kwao katika kuuhami Uislamu, wakajitolea kwa hali na mali, wakapoteza wazazi wao na watoto wao, mambo ya kupeana naseehah katika Dini na kuwa na Imani thabiti na yakini isiyokuwa na shaka yoyote, (yote hayo) yatategemea

© Quran wa Sunnah Society of East Africa – E-books 2005. www.qssea.net
uaminifu wao na mtu kuwa na imani ya uadilifu na wema kwenye sifa zao. Na italazimu yakwamba wao walikuwa ni wabora wa wale waliopewa ijaza na kibali cha uhakikisho kutokana na uaminifu na mategemeo yao kutoka kwa watu wote watakaokuja baada yao milele na milele."

Kisha akapokea riwaya yenye silsila iliyotoka kwa Abu Zur'ah, aliyesema: "Ukimuona mtu yoyote mwenye kuwatafutia kasoro maswahaba wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (*Sallallaahu 'alayhi wasallam*), basi jua yakwamba huyo ni mzushi (*zindeeq*). Hii ni kwa sababu kulingana na vipimo vyetu sisi, Mtume wa Mwenyezi Mungu (*Sallallaahu 'alayhi wasallam*) ni mkweli, na Qur'ani yasema kweli. Na waliotuletea sisi hii Qur'an na Sunan (kwa wingi ni Sunnah) ni maswahaba wa Mtume wa Mwenyezi Mungu. Wanachotamani wao ni kuwaumbua na kuwaporomosha mashahidi wetu ili waweze kukibatilisha Kitabu na Sunnah, haliyakuwa wao ndiwo wenye kustahiki kuumbuliwa kwani wao ni wazushi wakubwa (*zanaadiqah*)."

Madh-hab ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa'ah kuhusu maswahaba imetuwama kati-na-kati baina ya ncha mbili za ushupavu (upande mmoja) na uzembe (upande mwengine). Ni kati-na-kati baina ya washupavu wapindanifu waliowainua waheshimiwa miongoni mwao na kuwaweka katika daraja yenye kumstahiki Mwenyezi Mungu au mitume Wake, na baina ya wazembe watovu wa adabu wenye kuwabughudhi na kuwalaani. Kwahivyo wao ni wa kati-na-kati baina ya wale waliozidi na wale wenye kasoro – wao wanawapenda wote na wamewaweka kila mmoja wao mahali anapolingana napo, ambapo wanapostahiki kuwepo, kulingana na vipimo vya wema na uadilifu. Kwahivyo wao hawawainui na kuwaweka mahali ambapo hawastahiki kuwepo, wala hawawadharau, na kuwapokonya mambo wanayostahiki kuwa nayo. Kwahivyo, ndimi zao daima huwa zimeroama kwa kuwataja kwa wema tu, kulingana na yenye kuwastahili. Na nyoyo zao zimejaa mahaba juu yao.

Na kitu chochote kilichosihi kuhusiana na utesi na kutofahamiana kuliko tokea baina yao (au miongoni mwa baadhi yao), hapo kuhusiana na suala hilo wao walikuwa ni Mujtahideen. Sasa emma walikuwa sawa na watapata thawabu kwa ijtihaad zao na malipo mema kwa kusihi ijitihadi yao au walikosea na kwahivyo watapata ujira wao kutokana na ijtihaad na kusamehewa makosa yao. Wala wao hawakusifika kwa sifa ya kutakasika na makosa, kwani wao walikuwa ni wana-adamu, nyakati nyengine walikuwa kwenye usawa na nyakati nyengine walikuwa kwenye makosa. Lakini kuna tafauti kubwa mno kwenye usawa wao ukilinganisha na usawa wa watu wengine, na ni uchache ulioje wa makosa yao ukilinganisha na makosa ya watu wengine? Na juu ya hayo yote wao wameahidiwa msamaha na radhi kutoka kwa Mwenyezi Mungu (*Subhaanahu wata'aalah*).

Vitabu vya Ahl-us-Sunnah vimejaa maelezo yenye kufafanua kanuni hizi zenye kudhihirisha utakaso kuwahusu watu hawa walio bora kabisa, wateule

© Quran wa Sunnah Society of East Africa – E-books 2005. www.qssea.net

miongoni mwa wana-adamu ili washirikiane na mbora wa walimwengu wote (*Sallallaahu 'alayhi wasallam*).

Mfano wa haya ni matamshi ya At-Tahaawee katika kitabu chake cha (kuhusiana na) 'Aqeedah ya Ahl-us-Sunnah: "Sisi twawapenda maswahaba wa Mtume wa Mwenyezi Mungu na wala hatupindukii mipaka katika kumpenda yoyote miongoni mwao, na wala hatujidhalilishi kwa yoyote miongoni mwao. Na tunamchukia kila mwenye kuwachukia wao au yoyote mwenye kuwataja kwa ubaya. Na wala hatuwataji wao isipokluwa kwa wema. Na kuwapenda wao ni katika Dini, Eemaan na Ihsaan na kuwachukia wao ni Kufr (ukafiri), Nifaaq (unafiki), na Tughyaan (dhulma)."

Amesema Ibn Abee Zayd Al-Qayrawaanee katika utangulizi wa kitabu chake mashuhuri Ar-Risaalah, alipokuwa akifafanua kanuni za Ahl-us-Sunnah: "Na zama zilizokuwa bora zaidi ni zile za wakati wa Mtume wa Mwenyezi Mungu. Na waliokuwa bora katika maswahaba ni makhalifa (wanne) waliokuwa juu ya uongofu, Abu Bakr, kisha 'Umar, kisha 'Uthmaan, kisha 'Alee, Mwenyezi Mungu awe radhi nao. Na wala asitajwe swahaba yoyote isipokuwa kwa wema. Ni imani yetu sisi kujiepusha na (kuzungumza kuhusu) tafauti ambazo zilizotokea baina yao. Na kwamba wao ndiwo wanaostahiki zaidi kutafutiwa udhuru miongoni mwa watu (na pia) dhana yetu juu yao iwe njema."

Imaam Ahmad Ibn Hanbal amesema katika kitabu chake As-Sunnah: "Na katika Sunnah ni kuzitaja sifa njema za maswahaba wa Mtume wa Mwenyezi Mungu – wote – na kujiepusha na (kuzungumza kuhusu) tafauti ambazo zilizotokea baina yao. Kwahivyo, yoyote mwenye kuwalaani maswahaba wa Mtume wa Mwenyezi Mungu au (hata) mmoja wao, basi huyo ni mzushi, Raafidhee. Kuwapenda wao ni Sunnah na kuwaombea wao du'aa (maombi) ni katika njia zenye kutukurubisha sisi na Allaah (taqarrub). Kuwaandama wao ndiyo njia na kuwaiga katika mifano yao ni katika wema..."

Na akasema: "Hairuhusiwi kwa mtu yoyote kuyataja makosa yao. Na wala hapana yoyote awezae kumkashifu yoyote miongoni mwao. Kwahivyo, yoyote atakaefanya hivyo, basi utawala (sultan) utawajibika kumkemea na kumuadhibu. Na badala ya kumsamehe, watalazimika kumuadhibu na kisha baadae wamshurutishe kuomba msamaha. Hapo akiomba msamaha, na amkubalie msamaha wake. Na iwapo hakuomba msamaha, na aanze tena kumuadhibu na kumuhukumu awekwe jela maisha mpaka atubie na abadilishe msimamo wake (kutoka katika imani yake ya upotofu)."

Imaam Abu 'Uthmaan As-Saaboonee akasema katika kitabu chake 'Aqeedat-us-Salaf wa As-haab-il-Hadeeth:
"Na wakakatikiwa yakwamba ni waajib kujiepusha na (kuzungumza kuhusu) tafauti ambazo zilizotokea baina ya maswahaba wa Mtume wa Mwenyezi Mungu na kuzitakasa ndimi zao katika kutaja chochote chenye kuleta ishara

© Quran wa Sunnah Society of East Africa – E-books 2005. www.qssea.net
za lawama au utwevu juu yao. Na wakakatikiwa yakwamba ni waajib kumuomba Mwenyezi Mungu Awarehemu wote na kuonyesha mapenzi juu yao."

Shaikh-ul-Islaam Ibn Taimiyyah amesema katika kitabu chake Al-'Aqeedat-ul-Waasitiyyah:
"Miongoni mwa misingi ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa'ah ni kuendelea kudumisha utakaso wa nyoyo na ndimi juu ya maswahaba wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (*Sallallaahu 'alayhi wasallam*), kama walivyosifiwa na Mwenyezi Mungu (*Subhaanahu wata'aalah*) aliposema (kama ilivyofasiriwa): **'Na walio kuja baada yao wanasema: Mola wetu Mlezi! Tughufirie sisi na ndugu zetu walio tutangulia kwa Imani, wala usijaalie ndani ya nyoyo zetu undani kwa walio amini. Mola wetu Mlezi! Hakika Wewe ni Mpole na Mwenye kurehemu.'** [Soorah Al-Hashr: 59:10]

Na (miongoni mwa misingi yao ni) utwiifu kwa Mtume kuhusu maneno yake: **"Musiwalaani maswahaba zangu! kwani naapa kwa yule ambae Aliyeimiliki nafsi yangu, lau kama mmoja wenu angelijitolea (kiwango cha) dhahabu (kilicho na) ukubwa wa mlima wa Uhud kwa njia ya sadaka, basi haitokuwa sawa na hata kipimo cha madd moja ya mmoja wao wala (hata) nusu yake."**

Na wao wamekubaliana na yale yaliyotajwa katika Qur'aan, Sunnah, na ijmaa'ah kuhusu wema waliokuwa nao (maswahaba) na daraja zao za juu. Na wakawapa upendeleo wale waliojitolea mali zao na wakapigana (kwa njia ya Mola wao) kabla ya ushindi kupatikana – makusudio ni mkataba wa al-Hudaybiyah – kuwazidi wale waliojitolea mali zao na kupigana baadae. Na wakawafadhilisha Muhaajireen kuliko Ansaar. Na wanaamini yakwamba Mwenyezi Mungu alisema kuwaambia wale waliopigana kwenye vita vya Badr – waliokuwa na idadi ya zaidi ya watu mia tatu: **'Fanyeni mutakalo, kwani Mimi tayari nishawasamehe.'**

Na wanaamini yakwamba hapana yoyote aliyekula kiapo (aliyembay'i) kwa Mtume (*Sallallaahu 'alayhi wasallam*) alipokuwa chini ya mti, atakaeingia motoni, kama alivyotuarifu Mtume (*Sallallaahu 'alayhi wasallam*). Kwa hakika Mwenyezi Mungu Alikuwa radhi nao na wao walikuwa radhi na Yeye. Na hapo walikuwa zaidi ya watu elfu moja na mia nne.

Wamemtaja kuwa ni mtu wa Peponi kila ambae aliyeshuhudiliwa na Mtume wa Mwenyezi Mungu yakwamba atakuwa Peponi, kwa mfano wale (maswahaba) Kumi, Thaabit Ibn Qays Ibn Shammas na wengineo.

Na wao wanathibitisha yale ambayo yaliyopokewa kwa njia ya tawaatur kutoka kwa Ameer-ul-Mu'mineen, 'Alee Ibn Abee Taalib (*Radhiallaahu 'anhu*) na wengineo yakwamba: Wabora wa Ummah huu baada ya Mtume wake ni Abu Bakr; kisha 'Umar. Kisha wakamueka 'Uthmaan kuwa wa tatu na 'Alee wa nne, Mwenyezi Mungu Awe radhi nao. Hii ni kama ilivyoashiriwa kwenye

© Quran wa Sunnah Society of East Africa – E-books 2005. www.qssea.net
athaar (riwaya zitokazo kwa maswahaba) na kama ilivyoafikiwa na kongamano yakwamba 'Uthmaan alikuwa ni bora (kuliko 'Alee) kwa kupewa uongozi (wa kuwa khalifah). Licha ya yote hayo, baada ya kuafikiana kwa umoja wao kuhusu ubora wa Abu Bakr na 'Umar, baadhi ya Ahl-us-Sunnah walihitilafiana kuhusu aliyebora baina ya 'Uthmaan na 'Alee. Kwahivyo pote mojawapo wakamuona 'Uthmaan kuwa anastahiki kisha wakatulia kimya na wakamuweka 'Alee kuwa ni (khalifah) wa nne. Na pote jengine wakamuona 'Alee kuwa ndiye anaestahiki. Na kukawepo na pote jengine ambalo likaamua kutochukuwa upande wowote. Lakini shauri walilokatikiwa nalo Ahl-us-Sunnah ni kumfanya 'Uthmaan kuwa ni bora kisha 'Alee. Lakini hiyo haijali kitu, kwani hili suala la 'Uthmaan na 'Alee si miongoni mwa misingi ambayo asiyekubaliana nayo awe mpotofu, kulingana na kundi kubwa (la wanavyuoni) wa Ahl-us-Sunnah. Bali, mas-ala ambayo mwenye kwenda kinyume nayo ni mpotofu ni kuhusu suala la khilaafah – nalo nikwamba wao (ni lazima) kuamini yakwamba anaestahiki kuwa Khaleefah baada ya Mtume wa Mwenyezi Mungu ni Abu Bakr, kisha 'Umar, kisha 'Uthmaan na kisha ni 'Alee. Na yoyote mwenye kuishambulia Khilaafah yoyote miongoni mwazo, basi huyo amepotea upotevu ulio mbali zaidi kuliko punda wa watu wake."

Kisha akataja yakwamba wao wana mapenzi na mahaba juu ya jamii ya nyumba ya Mtume wa Mwenyezi Mungu na kwamba wao wanauhifadhi wasiya (wa mwisho) aliotuwachia Mtume wa Mwenyezi Mungu kuwahusu wao. Na kwamba wao wana mapenzi ya hali ya juu kuwahusu wakeze Mtume wa Mwenyezi Mungu, Mama Zao Waumini na kuamini yakwamba wao watakuwa ni wakeze kesho siku ya Kiyama. Kisha akasema:

"Na wakajitenga mbali kabisa na njia ya Rawaafidh – wale wenye kuwachukia maswahaba na kuwalaani – na mbali na njia ya Nawaasib – wale wenye kuwabughudhi jamii ya nyumba ya Mtume wa Mwenyezi Mungu – kwa maneno au kwa vitendo. Na hujiepusha na (kuuingilia ndani) utesi uliotokea baina ya maswahaba. Nao husema: Riwaya hizi, zilizopokewa kuhusu makosa yao, hupatikana miongoni mwake, mambo ambayo si ya kweli, mambo yaliyo ongezwa urongo, matukio fulani yaliyotengwa, na yale ambayo yaliyobadilishwa kutoka kwenye hali yake ya asili. Ama kuhusu yale ambayo ni saheeh miongoni mwake, basi yote yenye kuhusu mas-ala hayo, wao (maswahaba) wamesamehewa – emma walifanya ijtihaad na wakawa wamepata au walifanya ijtihaad na kukosea. Na juu ya hayo, wao hawaamini yakwamba kila mmoja wao ametakasika na makosa na kuwa hawatendi madhambi makubwa wala madogo. Bali, wanaweza kutenda madhambi kwa ujumla, lakini kutokana na fadhla na wema waliokuwa nao, wao hawana budi kusamehewa (madhambi ya) aina yoyote waliyo yafanya – iwapo wamefanya (hayo madhambi). Jambo hili limefikia kiwango cha kupata msamaha wa mambo maovu ambayo hata wale watakaokuja baada yao hawatoweza kusamehewa kwa kufanya madhambi mfano wake. Sababu ni kwamba wao wana amali njema ziwezazo kufutilia mbali amali mbovu, mfano ambao hautopatikana na waliokuja baada yao.

© Quran wa Sunnah Society of East Africa – E-books 2005. www.qssea.net

Imethubutu kutokamana na hadeeth ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (*Sallallaahu 'alayhi wasallam*) yakwamba wao ni wabora kuliko vizazi vyote na kwamba lau mmoja wao angelijitolea mudd moja (ya dhahabu) kwa njia ya sadaka itakuwa ni bora kuliko mlima mzima wa Uhud wa dhahabu wa wale watakaokuja baada yao. Zaidi ya hayo, ikiwa kwa mfano mmoja wao alifanya madhambi, basi emma alitubia kwa madhambi hayo, au alifanya amali fulani ambayo iliyofutilia mbali madhambi hayo. Au alisamehewa madhambi hayo kutokana na wema wa utangulizi wao au kwa kushufaiwa na Muhammad (*Sallallaahu 'alayhi wasallam*), ambayo maswahaba ndiwo wenye haki zaidi miongoni mwa watu katika kupata shifaa' hiyo. Au labda, aliwahi kukumbwa na mitihani ya hapa ulimwenguni, ambayo atapata malipo kwa ajili hiyo. Sasa ikiwa hayo yote ni kwa ajili ya madhambi yaliyotendwa (na wao), kisha huwaje kuhusu mas-ala ambayo waliyoyafanyia ijtihaad? Ikiwa wamepata (katika ijtihaad yao) watakuwa na malipo mara mbili na ikiwa wamekosa (katika ijtihaad yao) watapata malipo mara moja na makosa yao watasamehewa.

Zaidi ya hayo, kiasi kilichoachwa, tena kikasamehewa kutokana na amali (mbaya) zilizofanywa na baadhi yao ni chembe ukilinganisha na wema wao na sifa zao njema, kama vile kumuamini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, Jihaad katika njia Yake, Hijrah, kuinusuru dini Yake, ilimu yenye manufaa, na amali njema. Na yoyote mwenye kusoma historia za watu (yaani: maswahaba) kwa utaalamu na mazingatio, na kuyasoma yale ambayo Mwenyezi Mungu aliyowabarikia nayo katika fadhla Zake, atakuja kutambua kwa yakini yakwamba wao walikuwa ni wabora wa viumbe baada ya mitume. Hawakuwahi kupatikana na wala hawatowahi kupatikana watu wa aina hiyo kama wao. Na (atakuja kutambua yakwamba) wao walikuwa ni safwah (wateule walio bora kabisa) kutokamana na vizazi vyote vya Taifa hili (la Uislamu), ambalo lenyewe ni bora na lenye heshima kubwa miongoni mwa mataifa yote mbele ya Mwenyezi Mungu."

Hii ni mifano mitano itokayo kwa Salaf As-Saalih (wema waliotutangulia) kuhusu yale yaliyotulazimu kuyaamini kuhusiana na wabora wa viumbe baada ya Mitume na Manabii. Kitu kimoja ambacho inatupasa kufahamu ni kwamba kuwaumbua watu hawa makhsusi na walio wateule kwa hakika ni kuiumbua Dini. Hii ni kwa sababu Dini (hii) haikufikilizwa kwa wale waliokuja baada yao isipokuwa kupitia kwao. Na ishatangulia kutajwa kwenye maneno ya Abu Zur'ah yakwamba: **"Waliotuletea sisi hii Qur'an na Sunan (kwa wingi ni Sunnah) ni maswahaba wa Mtume wa Mwenyezi Mungu. Wanachotamani wao ni kuwaumbua na kuwaporomosha mashahidi wetu ili waweze kukibatilisha Kitabu na Sunnah, haliyakuwa wao ndiwo wenye kustahiki kuumbuliwa kwani wao ni wazushi wakubwa (*zanaadiqah*)."** Haya yanawahusu wale wenye kuwakosea heshima yoyote miongoni mwa maswahaba. Na inaonyesha yakwamba yoyote mwenye kumkosea heshima swahaba haimdhuru hata chembe bali yote hayo ni yenye kuwafaidisha wao, kulingana na hadeeth iliyotangulia hapo awali ya **"mtu aliyefilisika."** Na inaonyesha yakwamba mwenye kuwavunjia

© Quran wa Sunnah Society of East Africa – E-books 2005. www.qssea.net

heshima anajidhuru yeye mwenyewe. Kwahivyo, yoyote anaekuwa na mapenzi yao, ndani ya moyo wake na ukosefu wa chuki juu yao, na akauhifadhi ulimi wake anapotaja chochote chenye kuwahusu wao isipokuwa kwa wema, basi huyo na amshukuru Mwenyezi Mungu kwa ne'ema hii. Na amuombe Mwenyezi Mungu amthibitishe juu ya uongofu huu. Na yoyote mwenye chuki juu yao kutoka katika moyo wake na ulimi wake ukawa haujizuii anapowataja wao kwa yale yasiyowafaidisha wao, basi huyo analazimika **kumcha** Mwenyezi Mungu na **akomeke** na uhalifu huwo. Na ni lazima **atubie** kwa Mwenyezi Mungu maadamu mlango wa toba uko wazi mbele yake, kabla hajajuta katika wakati ambao majuto hayatokuwa na manufaa.

Ewe Mola wetu usizifanye nyoyo zetu zikapotoka baada ya kutuongoza na kutupa rehema zitokazo Kwako, kwa hakika Wewe ndiye mpokezi wa maombi yote. **"Mola wetu Mlezi! Tughufirie sisi na ndugu zetu walio tutangulia kwa Imani, wala usijaalie ndani ya nyoyo zetu undani kwa walio amini. Mola wetu Mlezi! Hakika Wewe ni Mpole na Mwenye." kurehemu.'**